Jumiko la Maliasili Tanzania

Tanzania Natural Resource Forum

**Wanyamapori kwa watanzania wote: Kusimamisha upotevu, kuendeleza raslimali na kupanua mafao**

# CHAPISHO NA. 2

## SABABU ZA KUPUNGUA KWA WANYAMAPORI TANZANIA

**MAMBO MUHIMU:**

⇨ **Tanzania imeonesha dhamiri imara juu ya uhifadhi wa wanymaapori na bioanuai ikitenga kiasia cha asilimia 30 ya ardhi kama maeneo yaliyohifadhiwa ambako makazi ya binadamu yamezuiliwa.**

⇨ **Hata hivyo hifadhi hizo na mapori ya akiba mara nyingi hayakidhi haja ya hifadhi ya wanyamapori katika maeneo husika. Spishi nyingi zinahitaji raslimali ambazo zinapatikana nje ya maeneo yaliyohifadhiwa katika misimu fulani kwa mwaka. Pia wanyama wengi wanaishi nje ya maeneo yaliyohifadhiwa wakati wote.**

⇨ **Uhifadhi hutegemea wanyamapori waliohifadhiwa ndani ya mipaka ya hifadhi na mapori ya akiba na pia nje ya maeneo haya katika ardhi za vijiji na ardhi binafsi.**

⇨ **Tanzania bado haijafanikiwa vizuri kuhifadhi wanyamapori walio nje ya maeneo yalioyohifadhiwa. Hii ni kwa sababu jamii na watu binafsi hawajaona motisha ya kuhifadhi wanyamapori. Kisheria maduhuli yaliyokusanywa huenda hazina na taasisi za serikali. Kiwango kidogo sana cha maduhuli hubakizwa au hurudishwa kwa jamii au watu binafsi.**

⇨ **Idara ya Wanyamapori pia ina upungufu wa raslimali unaosabibishwa na mfumo huo wa kugawana mapato.**

⇨ **Ili wanyamapori wahifadhiwe ni lazima kisheria kuwepo thamani ya kiuchumi kwa jamii ambayo ndiyo yenye maamuzi juu ya matumizi ya raslimali zilizo katika ardhi zao.**

⇨ **Sekta binafsi na vyama huru ni budu kutoa mchango katika uandaaji wa viwango, matendo ya kiusimamizi na mifano ya biashara bunifu kwa uratibu na Idara ya Wanyamapori.**

*Kwa kushirikiana na*

policy forum

WILDLIFE CONSERVATION SOCIETY

WWF

Pastoralists Indigenous Non Governmental Organizations Forum PINGO's FORUM

*© JMT 2008*

## Kwanini wanyamapori hupungua Tanzania?

Inaweza kushangaza kuwa idadi ya wanyamapori Tanzania wanapungua wakati Tanzania imepata mafanikio makubwa katika uhifadhi wa wanyamapori. Tangu uhuru, miaka 47 iliyopita Tanzania imepanua maeneo ya ardhi iliyohifadhiwa kwa ajili ya wanyamapori, bioanuai na ulinzi wa mazingira. Na katika kipindi hichohicho idadi ya watanzania imeongezeka mara tano kutoka watu milioni 8 hadi watu milioni 38. Ongezeko la watu linamaanisha ardhi zaidi inahitajika kwa ajili ya kilimo, malisho na makazi na bado kuna ongezeko la mahitaji ya maliasili – ikiwemo mkaa, nyama za porini na mazao ya mbao. Changamoto zilizopo katika kuhimiza maslahi endelevu na kufikia usimamizi endelevu wa maliasili zimechangiwa na utendaji dhaifu katika upangaji wa matumizi bora ya ardhi.

Leo hii Tanzania imetenga asilimia 30 ya ardhi yake kama maeneo yaliyohifadhiwa ambako watu wamezuiliwa kuishi. Mataifa machache duniani yameweza kufanya hivyo. Kama Kielelezo Na. 1 kinavyoonesha Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba yamepanuliwa mfufulizo tangu uhuru.

*Kielelezo Na. 1: Upanuzi wa baadhi ya Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba Tanzania, 1964-2004*




*Chanzo: World Database of Protected Areas, World Conservation Monitoring Centre 2005*

**Lakini leo hii wanyamapori wanapungua licha ya Tanzania kuwa imetenga asilimia kubwa ya ardhi yake kama maeneo yaliyohifadhiwa. Kwa hiyo tatizo ni nini?**

## Wanyamapori nje ya hifadhi na mapori ya akiba

Sehemu ya kwanza muhimu ya maelezo ni kwamba katika maeneo mengi duniani hifadhi na mapori ya akiba siku zote havikidhi haja kwa uhifadhi wa wanyamapori katika eneo husika. Sababu ni kwamba maeneo hayo hayajitoshelezi. Wanyamapori huondokea nje ya mipaka ya maeneo yaliyohifadhiwa mara nyingi kwa sababu raslimali kama chakula na maji hupatikana nje ya maeneo hayo. Kama wanyamapori wangeweza kubaki ndani ya mipaka ya hifadhi na mapori ya akiba mathalani kwa kuweka uzio wa kuwazuia wanyama ndani, idadi ingepungua haraka. Hii ni kweli kwa wanyama wanaohama kama vile nyumbu na tembo. Kwa kawaida wanyamapori huhitaji maslahi ya kiikolojia kipindi fulani cha mwaka ambayo hupatikana nje ya mipaka ya hifadhi kama vile nyanda za malisho, maji, maeneo ya kupumzikia na maeneo ya kuzalia.

*Kwa mfano:*

⇨ Hata kama Pori la Akiba la Selous ndiyo eneo kubwa lililohifadhiwa Afrika, karibu kilomita za mraba 50,000; miondoko ya tembo huenda nje ya eneo la hifadhi kwa pande zote ikifikia takribani kilomita za mraba 100,000.

Kaskazini mwa Tanzania spishi kama nyumbu, pundamilia na jamii ya swala huhama maeneo makubwa kila mwaka kati ya maeneo yenye maji ya kudumu kipindi cha kiangazi na maeneo yenye malisho mazuri kipindi cha masika.

*Kwa mfano:*

⇨ Katika Hifadhi ya Taifa Tarangire wanyama huhama hifadhi kipindi cha masika na kutawanyika kwenda kaskazini, mashariki na kusini mwa hifadhi katika ardhi ndani ya mipaka ya vijiji mbalimbali Wilaya za Monduli, Simanjiro na Kiteto. Hifadhi ya Tarangire hutoa asilimia ndogo (chini ya asilimia 20) ya eneo lote la ardhi na makazi ambayo wanyamapori wanahitaji kwa kipindi cha mwaka.

⇨ Hata Serengeti ambako Mapori ya Akiba matatu, Hifadhi moja ya Taifa, na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro hutoa kama kilomita za mraba 30,000 za ardhi iliyohifadhiwa, wanyamapori bado hutumia maeneo muhimu nje ya maeneo ya hifadhi katika Wilaya ya Ngorongoro (Tarafa ya Loliondo) na katika Wilaya za Serengeti na Tarime katika kipindi cha uhamaji wa nyumbu katika mwaka.




***Kutokana na wanyamapori kutumia maeneo makubwa, uhifadhi hutegemea wanyamapori waliohifadhiwa <u>ndani</u> ya hifadhi na mapori ya akiba na <u>nje</u> ya maeneo haya katika ardhi za <u>vijiji</u> na watu binafsi.***

**Kisanduku Na. 1: Mapori Tengefu ni nini?**

Mapori Tengefu (GCA) wakati fulani hurejewa kama maeneo yaliyohifadhiwa lakini kuyaita Mapori Tengefu yamehifadhiwa inachanganya kwa sababu hayatoi ulinzi wowote kwa wanyamapori. Mapori Tengefu yalianzishwa wakati wa ukoloni kama maeneo yaliyotengwa ambako wanyama wasingewindwa bila leseni. Mapori Tengefu hayajawahi kudhibiti makazi au shughuli zingine za kibinadamu ndani ya mipaka na hivyo kutotoa ulinzi kwa makazi ya wanyamapori. Chini ya Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 1974 popote Tanzania hakuna wanyama wanaoweza kuwindwa bila leseni hivyo Mapori Tengefu hayana maana—hayatimizi kusudi lolote kwa vile wanyama popote pale Tanzania hawawezi kuwindwa bila leseni.

Mapori ya Akiba yanatofautiana sana na Mapori Tengefu. Katika Mapori ya Akiba watu hawaruhusiwi kuishi wala kufanya shughuli za kiuchumi bila kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori. Vilevile katika Hifadhi za Taifa uvunaji wa maliasili umezuiliwa kabisa na uwindaji hauruhusiwi. Uwindaji unaruhusiwa katika Mapori ya Akiba kwa msingi wa kupewa kiasi cha wanyama na leseni kama ilivyo mahali popote pale nchini.

Mapori Tengefu hayatoi ulinzi wa maana kwa makazi ya wanyamapori isipokuwa tu katazo la uwindaji wa wanyamapori ambao unazuiliwa mahali popote Tanzania. Katika tathmini ya sekta ya wanyamapori ya mwaka 1995 Mapori Tengefu hayakuonesha kuwa na tija yoyote kwa kuchangia uhifadhi wa wanyamapori. Sera ya Wanyamapori Tanzania ya mwaka 1998 ilipendekeza Mapori Tengefu ama yapandishwe kuwa Mapori ya Akiba au yabadilishwe kuwa maeneo ya hifadhi za jamii ambako haki ya kutumia wanyamapori ingetolewa na faida ya wanyamapori katika ardhi za vijiji ingeonekana.

Kama wanyamapori wana gharama zaidi kuliko faida kwa wanavijiji hivyo wanavijiji watafanya kila wawezalo kuwaondoa wanyamapori ili waweze kuboresha maisha yao na ustawi wa familia zao. Kwa mfano watapanua mashamba na kuharibu makazi ya wanyamapori kwa sababu kilimo kina faida na wanyamapori huleta hasara.

⇨ Usimamizi wa sasa wa wanyamapori Tanzania hautoi mifumo yenye tija kwa kuwezesha jamii zifaidike kisheria kutokana na wanyamapori.

*Kwa mfano:*

⇨ **Kuna biashara kubwa inayokua ya nyama za porini katika maeneo mbalimbali nchini.** Mfano, Mikoa ya Kigoma, Kagera na Mara ambako jamii wanafaidika kwa kiwango kikubwa ingawa **sio kwa halali** kutokana na wanyamapori. Kwa sababu uwindaji wa wanyamapori ni haramu lakini jamii haina motisha wa kudhibiti uvunaji wa wanyamapori na hakuna mifumo saidizi ya kuwezesha kutimiza azma hiyo. Matokeo yake uwindaji nyama za porini umekuwa na athari kubwa kwa idadi ya wanyamapori. (Chanzo: TRAFFIC, 2000 na 2007)

Kwa hiyo, kama tathmini ya sekta ya wanyamapori ya mwaka 1995 na Sera ya Wanyamapori Tanzania ya mwaka 1998 (toleo lililorekebishwa 2007) vinatambua kuwa ili wanyama wadumu Tanzania lazima mwenendo wa sasa ubadilishwe, ni lazima wanyamapori wawe na thamani kwa jamii, na jamii inahitaji kuwa na uwezo wa kusimamia wanyamapori kama vile wanavyosimamia mifugo, kilimo, misitu, na maliasili nyingine katika ngazi ya kijiji.

Hivyo mafao ambayo wananchi wanaweza kupata kutoka wanyamapori yanaweza kuwa kwa njia nyingi: uvunaji wa nyama endelevu, mapato kutoka kwa biashara za wanyamapori kama vile upigaji picha na uwindaji, ajira ikiwemo uanzishaji wa ujasiriamali unaoendana na utalii wa wanyamapori.

Wanyamapori wana faida na jamii ina fursa nyingi za kutafuta maslahi kutokana na wanyamapori ikiwa wanapata haki sawa za kusimamia wanyamapori na kupokea mapato.

*Kwa mfano:*

⇨ Utafiti wa serikali wa kiuchumi unaonesha kuwa matumizi ya wanyamapori (uwindaji, ukamataji wanyama hai na mapato mengine ya kiuvunaji) yalitoa mapato ya shilingi bilioni 15.3 (dola milioni 13) mwaka 2006, bila kuhesabu kiasi kikubwa cha mapato yaliyokusanywa kutoka kwa utalii wa kupiga picha Serengeti na Hifadhi zingine za Taifa.

Mgao dhaifu wa matumizi, faida na haki za kusimamia wanyamapori kwa jamii ni sababu za msingi za kupungua kwa idadi ya wanyamapori. Bado wanajamii hawajaona motisha za kuhifadhi au kulinda wanyamapori nje ya maeneo ya hifadhi na mapori ya akiba.

***Licha ya mwongozo sahihi wa tathmini ya sekta ya wanyamapori ya mwaka 1995 na Sera ya Wanyamapori Tanzania (toleo lililorekebishwa mwaka 2007), usimamizi wa wanyamapori kijamii bado haujatekelezwa vizuri – ikiwa na madhara kwa wanyamapori nchini.***

*Tembo (Loxodonta africana) katika mfumo ikolojia wa Tarangire*